

## Kuvuna

- Viazi vitamu hukomaa baada ya miezi 4 tangu kupandwa.
- Viazi huvunwa kwa kutumia jembe la mkono.
- Uvunaji hufanyika kwa kuchimba, kung'oa shina lote au kutoa baadhi ya viazi na kuacha shina liendelee pale shambani.



*Viazi lishe vilivyo tokana na mbegu bora*



*Mtafiti akikagu viazilisho vilivyo tokana na mbegu bora*




*Mkulima akifurahia mavuno ya viazi lishe vilivyo tokana na mbegu bora.*

## Usindikaji na masoko

- Usindikaji huongeza thamani na fursa za masoko.
- Inashauriwa kusindika viazi vitamu ili kupata unga bora ambao hutumika kutayarisha mapishi mbalimbali kama vile **uji, ugali, chapati, maandazi, keki, biscuit na tambu.**



*Unga bora wa viazi lishe*



## KILIMO BORA CHA VIAZI VITAMU



*Kimetayarishwa na:*

*Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania  
TARI - Naliendele  
S. L. P. 509,  
Mtwara*

*July, 2019*

## KILIMO BORA CHA VIAZI VITAMU

### Utangulizi.

Viazi vitamu ni miongoni mwa mazao muhimu ya chakula nchini Tanzania. Zao hili hustawi karibu mikoa yote hapa nchini Tanzania. Kwa uzalishaji, viazi vitamu vinashika nafasi ya nne baada ya Mahindi, Muhogo na Maharage. Viazi vitamu pia vinashika nafasi ya tatu kwa umuhimu baada ya Muhogo na viazi mviringo kwa mazao ya chakula aina ya mizizi na jamii ya viazi.

### Mazingira ya ustawishaji

- Viazi vitamu hustawi vinzuri kwenye udongo tiftufu, wenye rutuba ya kutosha na unaoruhusu maji kupenya kwa urahisi.
- Udongo wa mfinyazi na wenye kokoto nyingi haufai kwani huzuia mizizi kupenya na kupanuka.
- Pia hustawi maeneo yenye mwinuko chini ya mita 1700 kutoka usawa wa Bahari.
- Huhitaji joto la kati ya nyuzijoto 15 -30.
- Huhitaji mvua ya wastani wa milimita 600 kwa mwaka.

### Kutayarisha shamba

- Fyeka na kung'oa visiki kisha tifua udongo vizuri kabla ya msimu.
- Andaa matuta vizuri ili kuongeza uzalishaji.

### Kuchagua mbegu bora za viazi vitamu

Inashauriwa kutumia mbegu bora zilizoainishwa kitaifa na Taasisi za utafiti wa kilimo kwa ajili ya kutumika katika kanda mbalimbali:

- Ukanda wa Pwani na kanda ya kati aina zinazofaa ni **Mataya, Kiegea, Chahwa, Simama na Ukerewe.**
- Kanda ya Ziwa na ile ya Magharibi ni **Ejumla, Naspoti 1, Sinia, Kakamega, Kabode, Polista na Jitihada.**



*Wakulima wakiandaa mbegu za tayari kwa kupanda*

### Kupanda viazi

- Panda kwenye matuta au kitalu kilicho pandishwa juu ili kutoa mavuno zaidi
- Umbali kutoka tuta hadi tuta ni sentimita 100 na kutoka mmea hadi mmea ni sentimita 30.
- Kwa uzalishaji wa mbegu, umbali kutoka tuta hadi tuta ni sentimita 100 na mmea hadi mmea ni sentimita 15.
- Viazi vitamu hupandwa kwa kutumia vipande vya shina linalo tambaa (vines) vyenye umri kati ya miezi 2-3
- Urefu wa mbegu ya kupanda inashauriwa iwe kati ya sm 15-25
- Upandaji unaostahili ni kufukia sehemu kubwa ya pingili ardhini kwa kulaza kidogo udongoni na kufukia.



*Wakulima wakipanda shamba la mbegu za viazi*

### Matumizi ya mbolea

- Inashauriwa kuchagua shamba lenye rutuba ya kutosha ili kupata mavuno mengi.
- Utafiti wa matumizi ya mbolea nchini Tanzania unaendelea kufanyika ili kuainisha mahitaji sahihi ya mbolea katika uzalishaji wa viazi vitamu.

### Palizi

- Palizi ifanyike mara 2-3 kwa msimu ili kuzuia magugu ambayo husababisha upotevu wa mavuno.
- Kurudishia udongo kwenye mashina wakati wa palizi huongeza mazao.
- Fukia mipasuko yote ya ardhi kwenye shamba la viazi vitamu ili kuzuia wadudu ambao huweza kingia na kuathiri ubora wa viazi.



### Visumbufu vya viazi vitamu

#### Magojwa

- Viazi hushambuliwa na magonjwa yanayotokana na virusi kama Sweet Potato Chlorotic Stunt virus (SPCSV), Fangasi kama (sweet potato Alternaria blight), kuoza shingo (Bacteria soft Rot), minyoo fundo (Root notes Nematodes), na uozo wa kahawia (Brown Rot).
- Njia kuu ya kudhibiti magonjwa huya ni kutumia mbegu bora zenye ukinzani na kuzingatia kanuni za kilimo bora cha viazi.

#### Wadudu waharibifu

- Vikongomwa wa viazi (weevils) ni wadudu wanaoshambulia kiasi kikiwa udongoni.
- Fukia mipasuko yote ya ardhi kwenye shamba la viazi vitamu ili kuzuia wadudu ambao huweza kingia na kuathiri ubora wa viazi.